
Mambo ambayo vijana wanapaswa kujua kuhusu

# USAFIRISHAJI HARAMU WA WATU KWA MADHUMUNI YA KINGONO NA KUTUMIWA VIBAYA

## Byashara ya wafanyi kazi ni nini?

Usafirishaji haramu wa watu kwa ajili ya kazi ni pale mtu **analazimishwa kufanya kazi au kutoa huduma kwa** kutumia **nguvu, udanganyifu, vitisho,** au **kumtisha**.


Wengi wa wanaokupa kazi nchini Marekani hawafanyi usafirishaji haramu wa watu kwa ajili ya kazi, lakini ni muhimu kujua dalili zake ili uweze kujilinda na kuwalinda wengine.



## Dalili 10 za Onyo

**Ikiwa mtu...**

- **Anakulazimisha kulipa** kodi au gharama nyingine za nyumbani;
- Anakulazimisha kufanya kazi **ili kulipa deni**, au deni lako **linaendelea kuongezeka;**
- **Anakulazimisha kufanya kazi** pahali ya kwenda shule;
- **Anadhibiti** usafiri wako, mahali unapoenda, na watu unaozungumza nao; **anakutenga** na marafiki na familia;
- **Anakutishia kukudhuru** wewe au wapendwa wako, au kupiga simu polisi au mamlaka ya uhamiaji ikiwa hutafanya wanachosema;
- **Anazuia mshahara wako** au **anakata gharama** kutoka kwenye malipo yako;
- Anakuomba au anakulazimisha kufanya kazi inayokuweka kwenye **kemikali hatari** au **mazingira ya kazi hatarishi;**
- **Anashikilia** pasipoti yako, nyaraka zako, pesa zako, au simu yako;
- Anakulazimisha **kuishi mahali pa kazi** katika **hali mbaya ya maisha,** mara nyingi pamoja na watu wengi;
- Anakulazimisha kufanya kazi **kwa saa nyingi** bila malipo ya kutosha au mapumziko ya kutosha ya kula, kunywa, kupumzika, au kwenda chooni.



## Usafirishaji haramu wa watu kwa madhumuni ya kingono hutokea wapi?

Usafirishaji haramu wa watu kwa ajili ya kazi na kutumiwa vibaya vinaweza kutokea katika **aina nyingi za kazi na maeneo ya kazi**, ikiwemo:

- Migahawa (Restaurants)
- Mashamba na viwanda
- Kazi za ujenzi na utunzaji wa mazingira
- Kazi zisizo rasmi au kazi zinazolipwa kwa pesa taslimu
- Kazi za usafi, kutunza nyumba, na matengenezo
- Kazi za kulea au kutunza watu



## Wauzaji haramu ni akina nani?

**Wauzaji haramu wa watu hawaonekani hatari kila wakati.** Wanaweza kuwa wanaokupa kazi, watu wanaotoa "kazi" mtandaoni, wapenzi, marafiki au rika, wanafamilia, au watu unaowafahamu kwa juu juu. Wanaofanya usafirishaji haramu wa watu mara nyingi hutoa ahadi ambazo hazionekani kuwa za kweli, na hujaribu kukudhibiti wewe, pesa zako, au nyaraka zako. Kumbuka, **watu wazima wengi ni salama**, lakini ni muhimu **kujua dalili za usafirishaji haramu wa watu** ili uweze kujilinda.

## Unawezaje kupata msaada ikiwa wewe au mtu unayemjua anaweza kuwa katika hali ya usafirishaji haramu wa watu kwa ajili ya kazi?



**Una haki,** na hizi ni hatua unazoweza kuchukua ikiwa haki hizo zinakiukwa.

- Zungumza na **mtu mzima wa kuaminika**.
- Piga simu **polisi** wa eneo lako au **911** katika hali ya dharura, au kuripoti mtu anayekunyanyasa au anayekutumia vibaya.
- Wasiliana na **Nambari ya Kitaifa ya Msaada dhidi ya Usafirishaji Haramu wa binadamu**. Ziko wazi saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki.

**Simu**: 1-888-373-7888 **Tuma ujumbe kunako:** 233733

**Zungumzo ya moja kwa moja (Live Chat)**: https://humantraffickinghotline.org/en/chat

refugees.org

The production of this material was supported by Grant #90RB0054 from the Administration for Children and Families (ACF). Its contents are solely the responsibility of the U.S. Committee for Refugees and Immigrants (USCRI) and do not necessarily represent the official views of ACF.

U.S. COMMITTEE FOR REFUGEES AND IMMIGRANTS